# KAZI NA WAJIBU WA MAAFISA WA SERIKALI WALIOCHAGULIWA

## MASENETA




*Jukumu la Seneta ni kutetea maslahi ya Kaunti*

## MWAKILISHI WA WANAWAKE




*Tangu uhuru, wanawake wamekua wachache sana katika Bunge; na sauti zao kutosikika*

**KUFANYA MABADILKO KAMILI KUTOKA ZAMANI**

Pamoja Tutetee Haki

TUME YA HAKI ZA BINADAMU KENYA

Pamoja Tutetee Haki

KENYA HUMAN RIGHTS COMMISSION

# Kazi na wajibu wa Maafisa wa Serikali Waliochaguliwa

Toleo lililorekebishwa
Machi 2014

ISBN: 9966-941-81-9

Kimechapishwa na:

Tume ya Haki za Binadamu Kenya (KHRC)
Mkabala na Valley Arcade, Barabara ya Gitanga,
Sanduku La Posta 41079, 00100 GPO, Nairobi, Kenya.
Simu: +254020-2106709 / 2044545/202106763
Nukunishi: +254 020-3874997
Barua pepe: admin@khcr.or.ke
Tovuti: www.khrc.or.ke

Sehemu zote za chapisho hili zinaweza kutolewa bure, mradi Tume ya Haki za Binadamu Kenya
Imeridhi.

© KHRC 2013

# Yaliomo

1.0 UTANGULIZI……………………...…………………………………….........................................................……………5

1.1 Maafisa wa Serikali Waliochaguliwa ....................................................................................................................................7

1.2 Uamuzi wa Malipo ya Maafisa wa Serikali Waliochaguliwa katika Serikali ya Kenya.................................................. 9

2.0 KANUNI YA MGAWANYO WA MADARAKA……………………………………………………………...……...……... 10

2.1 Vithibiti na visawishaji kupitia matawi matatu ya serikali ..............................................................................................12

2.2 Kazi muhimu za Watunga sheria wote - Kikanda, Kitaifa, Seneti na Bunge la Kaunti: ……..........................................13

2.3 Kazi na wajibu wa wabunge katika ngazi ya kikanda- Jumuiya ya Afrika Mashariki....................................................18

2.2.1 Mwakilishi wa eneo Bunge katika Bunge la Kitaifa (MPs) ......................................................................................... 20

2.2.2 Mwakilishi wa Wanawake kwa Bunge la Kitaifa (MPs) ...............................................................................................22

2.2.3Maseneta…………………………………………….........................................…………………………………….24

2.3.1Wawakilishi wa Kaunti....................................................................................................................................................27

3.0 MAAFISA WA SERIKALI WALIOCHAGULIWA KATIKA SERIKALI KUU YA KITAIFA............................................ 29

4.0 MAAFISA WA SERIKALI WALIOCHAGULIWA KATIKA SERIKALI YA KAUNTI …......................….......……….... 34

4.1 Kazi ya Gavana na Naibu wa Gavana.…………………..……………………….............................................……………..…..34

5.0 MAJUKUMU / KAZI ZA RAIA………......……….............................................……………………………………..38

# Shukrani

Tume ya Haki za Binadamu Kenya (KHRC) inashukuru zaidi Mashirika ya Jamii ya Haki za Binadamu (HURINETs) zinazoendelea kusisitiza kuwa kuna pengo la maarifa juu ya nini hasa wanachofanya wanasiasa, ni kiasi gani wanachopata na hivyo, ukosefu wa kigezo madhubuti cha kupima utendaji kazi wao.

Ari ya kuziba pengo hili ndilo lililohamasisha chapisho hili. Tunatumaini kwamba itashawishi shauku ya wasomaji ya jinsi gani serikali katika ngazi ya kaunti na kitaifa zinavyofaa kuendesha na kuchangia ushiriki wa raia ambao sasa ni haki na wajibu ulioainishwa katika katiba ya Kenya. Ni matumaini yetu kwamba chapisho hili litakuwa na manufaa kwa wakaguzi wa kijamii na wakufunzi wengine katika kutambua wajibu wa waliobeba jukumu na jinsi wanavyopaswa kuwajibika kwa kazi zipi.

KHRC inamshukuru sana Nduta Kweheria ambaye aliukubali wito wa kukusanya huu uchapisho ulio mpana na rahisi pia. KHRC pia inawashukuru Grace Mutung'u, Davis Malombe, George Morara, Peter Kibiru, Lillian Kantai, Bill Mureithi, Vincent Musebe, Jamilla Wahome na Beryl Aidi, Samuel Oyomo, Charles Ouma na Grace Were kwa mchango wao kwa uhariri wa muhtasari huu.KHRC pia inamshukuru Mathias Botany na Wilson Njenga kwa kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili na kuhariri chapisho hili.
Hatimaye, lakini kwa vyovyote vile si mwisho, KHRC inatoa shukrani kwa Ubalozi wa kifalme wa Norwei (RNE) kwa kusaidia chapisho la kwanza lanakala hii Machi 2013,Shirika la Msaada la Kikristo,Nairobi waliopiga chapa nakala hii April 2013 na Waendeshaji wa Mpango wa Uajibikaji(DAP) waliosaidia kwa uchapishaji wa toleo la pili lililorekebishwa Machi 2014.KHRC inathamini uendelezi wa msaada kutoka mashirika yao katika nyadhifa tofauti.

# Kuhusu KHRC

Tume ya Haki za Binadamu Kenya (KHRC) ni Shirika lisilo la Kiserikali (NGO) lililoanzishwa mwaka wa 1992. Tangu uanzilishi wake, KHRC imefanya kazi kwa kuelekeza kukita haki za binadamu na misingi ya demokrasia katika Kenya. Tume ya KHRC ni tofauti na Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu (KNCHR) ya Serikali ambayo ilianzishwa mwaka wa 2003.

KHRC ina mikakati na mchakato wa kujiongoza katika kufanikisha Dira: Haki za binadamu kwa nchi na jamii; Dhamira: Kuendeleza haki za binadamu, maadili ya kidemokrasia, heshima ya binadamu na haki ya kijamii; na kwa kufanya kazi kuafikia Lengo la: kuimarishwa kwa haki za binadamu zinazozingatia utawala bora katika ngazi zote.
Malengo muhimu ya KHRC katika kipindi cha 2013-18 yatakayotekelezwa kwa mipango nne yaani: -

i) Haki na Utawala;
ii) Usawa na Kutobagua;
iii) Haki za Kiuchumi na Jamii; na
iv) Maendeleo ya Kishirika na Taasisi endelevu.

### Kazi Yetu

KHRC ina historia ndefu ya uwezo na mshikamano kamilifu katika kukabiliana na haki mbalimbali za binadamu na masuala ya ukiukaji katika ngazi mbalimbali za jamii. Hili limefanikiwa kwa utumishi wa mbinu za haki kwa utafiti; harakati za kujenga ushirikiano wa kijamii; nyaraka za ukiukwaji wa haki za binadamu, uchechemuaji wa ushahidi na utetezi.

KHRC imekuwa na uwezo wa kutambua sehemu za kiingilio za haki za binadamu na kutoa uongozi wa kitaalamu unaohusisha mfumo wa haki za binadamu kwa sekta mbalimbali katika jamii na hivyo kupanua mjadala wa wafuasi wa haki za binadamu. Mashuhuri ni kuwa, KHRC imekuwa kipao mbele kwa uanzilishi wa kazi ya kushughulikia maisha na haki za kazi, masuala ya wasagaji; ukaguzi wa kijamii kupitia Manifesto ya Watu na Mipango ya Alama; mageuzi ya kikatiba, uchaguzi tawala ;na masuala ya haki ya mpito yote kutokana na mtazamo wa haki za binadamu.
KHRC pia imekuwa katika harakati za kueneza haki za binadamu kwa kukuza Mashirika ya jamii ya Haki za Binadamu (HURINETs) na kuatama mashirika machanga ya kutetea haki za binadamu katika ngazi zote; na kufanya kazi na mitandao mingi, miungano na majukwaa mengine katika ngazi za ndani, kitaifa, kikanda na kimataifa.

Kudumu kwa mafanikio ya KHRC ni sifa inayotokana na watumishi wenye ashiki sana, wenye uwezo na nidhamu mbalimbali za haki, nia ya na uwezo wa kukabiliana na matukio mbalimbali na mifumo ya ukiukaji wa haki za binadamu katika jamii. Kwa njia ya kazi zake, KHRC kwa kiasi kikubwa imechangia uzalishaji wa bwawa la kitaifa na kimataifa la wafanyakazi wanaotambulika kwa haki za binadamu na wasomi ndani ya nyanja ya utawala na haki za binadamu.

Hatimaye, KHRC imepata mafanikio yake kupitia utawala mzuri wa shirika na ufanisi katika Ufuatiliaji na Mifumo ya Tathmini (M & E) ambayo inajitahidi mara kwa mara kuboresha.

# 10. Utangulizi




*Raia wakiandamana kupinga kutowajibika. Asili:KHRC*

Katika miaka 50 ya uhuru wa Kenya na uchaguzi kumi kwa ujumla, haijawahi kuwa wazi kwa raia wengi nini hasa kazi ya Wabunge na wamiliki wengine waliochaguliwa ofisi.

Mwaka wa 2007, Manifesto ya watu ya KHRC na Mpango wa Alama uliwekezwa kwa nguzo ya kwamba Manifesto ya vyama vya siasa na ahadi za utendaji wa maendeleo wao haukuwa na maana sana kwa wapiga kura bali kuwa ni rangi zakutengenisha kundi moja la wapiga kura kutoka kwa lingine na zaidi kwa mtazamo wa kikabila badala ya itikadi[1]. Mambo mawili makubwa yameangazia pengo hili la ufahamu wa umma kwa majukumu na wajibu wa wale waliochaguliwa.

Uchaguzi wa 2013 kwa uhakika ndio wa kwanza kufanyika chini ya katiba mpya ilioidhinishwa rasmi mwezi wa Agosti 2010. Katiba imeunda nafasi sita za kujazwa kupitia kuweka alama karatasi sita za kupiga kura. Hili ni ongezeko kutoka nafasi tatu za uchaguzi zilizokuwepo tangu uhuru. Ripoti ya uangalizi wa uchaguzi wa KHRC ya Februari 2013 ambayo pia iliangalia ufahamu wa watu wa nafasi za kuchaguliwa za Kikatiba (iliochapishwa 3 Machi 2014 ) ilionyesha kwamba zaidi ya asilimia 80 % ya wananchi hawajui au hawana uhakika kuhusu kiwango cha mipaka ya uchaguzi . Zaidi ya hayo, zaidi ya asilimia 70% hawawezi kueleza wazi majukumu ya Rais licha ya nafasi hii ya kuchaguliwa kuwepo tangu uhuru;na chini ya asilimia 25% wako na ujasiri wa kujua kazi za wanaomiliki nafasi zingine za kuchaguliwa : - Seneta (asilimia 13%) ,Mwakilishi wa wanawake ( asilimia 15%), Gavana (asilimia 24%) na Mwakilishi wa Kaunti (asilimia 16%). Hili pia limeonekana kupitia uchunguzi wa mashirika mengine ya kiraia[3].

Hii imefanywa ngumu zaidi na uhakika ya kwamba kwa mara ya kwanza,Katiba inahitaji wapiga kura kuangalia uadilifu na uwezo wa viongozi waliowateua kwa ofisi pamoja na ukweli kwamba uchaguzi wa kitaifa wa Machi 2013 inasanjari na Kenya kuwa na washukiwa watatu wanaokabiliwa na mashtaka katika Mahakama ya Jinai ya Kimataifa (ICC).

madai ya uhalifu wa jinai dhidi ya ubinadamu ambayo yalitokea wakati wa uchaguzi mkuu wa 2007. Kumekuwa na mjadala mkubwa wa umma iwapo wale waliofunguliwa mashitaka na ICC wameafikia viwango vya uadilifu kwa maafisa wa serikali waliochaguliwa au kama watakuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yao na wakati huo huo kuhudhuria kesi kule ICC mjini Hague

1 Nduta Kweheria,Manifesto ya Wapiga Kura ni Muhimu kwa Uwakilishi halisi,Gazeti la Nation,Novemba 3,2007,uk 14
2 Kuhesabu muda hadi Uchaguzi wa Machi 2013:Ripoti ya Muda ya Uangalizi wa Kura,KHRC,2013 http://www.khrc.or.ke/resources/publications/doc_download/52-countdown-to-the-march-2013-general-elections-interim-election-report.html

Pili, Bunge la kumi (2008 na 2013) walifurahia mishahara na marupurupu kiasi cha Ksh 851, 000 kwa mwezi, wakati mapato kwa utaji wa Kenya ilikuwa chini ya Ksh2, 000 kwa mwezi (Yaani mara 425 chini ya malipo ya wabunge kila mwezi na kima cha chini cha malipo cha Ksh4, 050 kwa mwezi; hivyo mara 210 chini ya malipo ya wabunge kila mwezi. Wabunge hao hao wa Bunge la 10 katika mwezi wa Oktoba 2012 walipitisha Muswada wa kujilipa wenyewe 'malipo ya kustaafu' zaidi ya Ksh 9 Milioni (USD 110,000)kwa kila mmoja kwa wabunge 210. Kama huu Muswada ungepita wakati huo, ingekuwa na maana kwamba kwa Ksh 2,000 kwa mwezi, ingechukua miaka 61 kwa Mkenya wa kawaida kupata Ksh9M ya bonasi ambayo wabunge walijipendekezea wenyewe.Zaidi ya bonasi, mapendekezo ya malipo ya kustaafu ya wabunge yalikuwa pamoja na hati za kusafiria za kidiplomasia kwa ajili yao na wapenzi wao, mazishi ya kitaifa na kuruhusiwa kuingia sehemu za watu mashuhuri wanapofika uwanja wa ndege. Pendekezo hili lilipingwa kupitia maandamano ya KHRC na mashirika mengine ya kiraia na kilio cha umma kwa vyombo vyote vya habari na hii ilisababisha Rais kuondoa bonasi hizo kwa nusu.

Aidha, Bunge hilo la Kumi lilimshawishi aliyekuwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Njeru Githae kuidhinisha (siku ya Januari 2, 2013) kutolewa kwa zaidi ya Ksh10 Bilioni kwao kwa mfumo wa hazina ya maendeleo ya maeneo bunge(CDF) ili kutekeleza miradi ya CDF ikisalia wiki nane tu kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Machi 4, 2013. Hii ilisimamishwa kupitia uamuzi wa mahakama[4].




*Waandamanaji nje ya jengo la Bunge Nairobi tarehe 9 Oktoba, 2012 baada ya watunga sheria kujipigia kura kupata $110,000 zaidi. Asili:CNN*

3 Tazama Ripoti ya Ugatuzi ya Kituo cha Africa cha Utawala Wazi(AfriCOG),Juni 2012 inayopatikana http://www.africog.org/reports/devolution iliangaliwa Machi 14,2013
4 Aridhihali nambari 71 ya 2013,kuhusisha uamuzi wa kikatiba wa kupeana Ksh.10.1 Bilioni kwa kamati ya uongozi ya CDF ili wabunge waweze kukamilisha miradi. Ona http://www.tisa.or.ke/uploads/Court-Order.pdf iliyoangaliwa Machi 14, 2013

Ukweli wa kwamba wengi wa wananchi hawajui mipaka ya uchaguzi au kazi ya wale wanaowachagua kuchukua ofisi inaonyesha kwamba i) wapiga kura hawaambatanishi uchaguzi na upatikanaji wa haki kwa njia ya upokeaji wa huduma ; ii) wapiga kura hawadhani kwamba ushuru wanaolipa unastahili kwa wao kudai kiwango fulani cha utendaji, ambayo ina maana kwamba wapiga kura wamekubali utendakazi usioridhisha kutoka kwa wale waliowachagua. Hii inapaswa kuwa sababu ya kushtusha; zaidi ya hivyo, wakati mtu anapouliza swali **"Kama si matarajio ya ubora na utoaji wa huduma kwa wakati, na utendaji kazi wa viongozi waliochaguliwa au kwa wapiga kura kupata thamani ya fedha zao (Kodi) , inayowafanya Wakenya kupiga kura katika uchaguzi mkuu, je nini?"** Kwa hakika hii ni sehemu inayohitaji masomo zaidi.

Nini hasa mamlaka, majukumu, wajibu au kazi ya wabunge (MPs) na maafisa wa serikali waliochaguliwa kuhudumu ili wapate malipo na faida wanazopata, na hata kufikiri wao wanahitaji zaidi?

Muhtasari huu unatoa maelezo mafupi ya majukumu mbalimbali ya maafisa wa serikali waliochaguliwa wanapaswa kufanya. Muhtasari huu umetengezwa kukabiliana na masomo[5] ambayo yalibainisha haja ya kujenga uwezo wa wabunge kuelewa na kutekeleza bora majukumu yao. Muhtasari huu pia unatambua haki ya na wajibu wa ushiriki wa raia ambao sasa unatambuliwa katika Katiba ya Kenya, 2010. Pia ina nia ya kuwasaidia wananchi kuelewa nini kazi ya kila mmoja wa maafisa wa serikali waliochaguliwa, kuwa na ufahamu wa kiasi gani yeye kama mlipa ushuru anamlipa kila afisa wa serikali aliyechaguliwa kutenda kazi na kuleta hamasa ya kwamba. Katiba inaruhusu raia kuwaita na kuwaondoa mamlakani maafisa wa serikali waliochaguliwa ambao hawatendi kazi zao kikamilifu (Kifungu 104) na kwenda kwa uchaguzi tena. Hatimaye, muhtasari huu unatoa wajibu ambao wananchi wanapaswa kuchukua ili kuhusika kama raia.

## 1.1 Maafisa wa Serikali Waliochaguliwa

Katiba ya Kenya (Kifungu 260) inatafsiri "Serikali", kama mujumuiko wa afisi , asasi na taasisi nyingine zinazojumuisha serikali ya Jamhuri chini ya Katiba. Katiba inaorodhesha maafisa wa serikali kwa kujumuisha afisi zote sita zinazomilikiwa na viongozi sita waliochaguliwa katika uchaguzi mkuu wa kwanza tarehe 4 Machi 2013 chini ya mfumo wa ugatuzi wa serikali kulingana na Katiba ya Kenya,2010. Hivyo basi,wanasiasa wote waliochaguliwa wanaotumikia serikali ya kitaifa-Rais,Naibu Rais,Seneta na wawakilishi wa Bunge la Kitaifa na serikali ya Kaunti-Gavana,Naibu Gavana na wawakilishi wa Bunge la Kaunti (MCAs) wote ni maafisa wa serikali.

Kifungu cha 73 cha Katiba ya Kenya kinatambua kuwa mamlaka yaliyopewa afisa wa serikali ni kwa imani ya umma kwa kutekelezwa katika namna ambayo (i) ni thabiti na kwa madhumuni ya malengo ya Katiba; (ii) inaonyesha heshima kwa watu; (iii) inaleta heshima kwa taifa na heshima kwa ofisi; na (iv) kukuza imani ya umma katika uadilifu wa ofisi. Katiba ya Kenya inampa afisa wa serikali jukumu la kuhudumia watu, badala ya nguvu ya kuwatawala.

Kanuni elekezi za uongozi na uadilifu ni pamoja na (a) uteuzi kwa misingi ya uadilifu binafsi, uwezo na uwepo, au uchaguzi huru na wa haki; (b) usawa na uadilifu katika maamuzi, na katika kuhakikisha kwamba maamuzi hayasukumwi na ubaguzi, upendeleo, dhamira zisizofaa au vitendo vya rushwa; (c) kujitolea kimsingi kwa maslahi ya umma, kuonyeshwa kupitia (i) uaminifu katika utekelezaji wa wajibu wa umma; na (ii) tamko la maslahi ya kibinafsi yanayoleta migogoro na wajibu wa umma; (d) uwajibikaji kwa umma kwa maamuzi na vitendo; na (e) nidhamu na kujitolea katika huduma kwa watu.

5 Uchunguzi Wazi wa Bajeti,2012,na Mpango wa Kuimarisha Bunge la Africa(APSP) ya kuangalia bajeti inayoendeleza faharasa ya Bunge la Africa(API) wamenakili kwamba kuna haja ya kujenga uwezo wa watunga sheria kufanya kazi yao vilivyo.Uchunguzi wa Wazi wa Bajeti ni huru kwa kuchunguza uwazi wa bajeti,uwajubikaji,na ushirikiano ulimwenguni.Ona http://www.internationalbudget.org iliyoangaliwa Machi 14,2013.



Afisa wa Serikali anafaa kuwa na nidhamu,katika maisha ya umma na rasmi, katika maisha binafsi, au katika muingiliano na watu wengine, kwa namna ambayo inazuia (a) mgongano wowote kati ya maslahi binafsi na kwa wajibu wa umma au rasmi; (b) kuacha maslahi yoyote ya umma au rasmi kwa ajili ya maslahi binafsi, au (c) kudhalilisha ofisi inayoshikiliwa na afisa.

Duniani kote , wananchi hupiga kura ili kuweka wanasiasa katika ofisi kama maafisa wa serikali . Kila raia ikiwa ni pamoja na watoto ,wasio na ajira, wagonjwa na wazee kisha hulipa ushuru kila wakati wao hununua bidhaa zozote (kama vile chakula , gesi ya kupikia au mafuta ya taa , sabuni nk), anapolipa nauli ya usafiri katika matatu au njia nyingine ya usafiri au anapolipia huduma ya maji, umeme au hata gharama za mitihani . Ushuru huu, ambao serikali unaita kama mapato yaliyokusanywa kutoka kwa raia wake kupitia kutoa fedha hutumika kulipa wale waliochaguliwa maafisa wa serikali na maafisa wote wa umma wanaoshiriki katika utoaji wa huduma kama polisi, maafisa wa gerezani na uchunguzi, maafisa wa leba na elimu, wahadhiri katika vyuo vikuu vya umma na vya kibinafsi, kilimo, maafisa wa mifugo na uvuvi, madaktari, wauguzi , wahasibu, majaji, mahakimu, mwendesha mashitaka na wanasheria wanaofanyia serikali kazi, wahandisi na makarani ) katika serikali za kitaifa na kaunti. Mapato yanayopatikana kutoka ushuru wa wananchi pia hutumika kufadhili miundombinu kama vile ujenzi wa shule , hospitali, barabara nk au kulipa mikopo serikali imechukua kujenga miundombinu iliyo na gharama kubwa kama vile barabara, reli, hewa na bandari ; na wa kufadhili utafiti na maendeleo ya kiteknolojia.

Ni muhimu kwamba kila nchi iwe makini juu ya uwiano wa mapato serikali hupata kila mwaka inavyotumika kulipa mishahara, ujenzi wa miundombinu mpya na kudumisha iliyopo, ununuzi wa vifaa muhimu (kama vile magari ya polisi, vifaa vya matibabu) na wasambazaji (kama vile madawa, mbolea na madawa ya wadudu) na kile hutumika kwa ajili ya utafiti na maendeleo. Wasiwasi umeonyeshwa juu ya mishahara mikubwa Kenya[6] , kama inavyo onekana kwa njia ya migomo mingi ya viwanda na maafisa wa umma kulalamika juu ya malipo duni, upungufu wa wahudumiaji na vifaa kwa taasisi za umma. Uchunguzi[7] umebaini kuwa licha ya Kenya kuwa juu kidogo tu ya Nchi Maskini zenye Madeni Makubwa (HIPC) kiasi; inalipa maafisa wa serikali waliochaguliwa wake juu sana kuliko vile Wabunge katika nchi zilizoendelea wanalipwa kama inavyoonekana katika takwimu ya SRC, KURASA ya 12.

Kuna tofauti kubwa kimalipo kati ya maafisa wa serikali waliochaguliwa Kenya ukilinganisha na raia wa kawaida anayelipa mishahara yao kupitia kulipa ushuru. Pato la pa capita ni 2000 kwa mwezi inayomaanisha kwamba Wabunge wanapata 400zaidi na rais 900zaidi kuliko raia wa kawaida anachopata kwa mwezi. Pamoja na Kenya kutegemea uchumi wa kilimo kwa kiasi kikubwa na kima cha chini cha sasa kuwa shilingi 4,350 kwa mwezi, wabunge wanapata 200zaidi na rais 400zaidi ya idadi kubwa ya wafanyakazi na wakulima wadogo walioajiriwa na sekta ya kilimo.

## 1.2 Uamuzi wa Malipo wa Maafisa wa Serikali Waliochaguliwa katika Serikali ya Kenya

Jedwali lililo chini linatoa muhtasari wa kiasi cha fedha walipa kodi hulipa viongozi kufanya kazi hizi katika muda wa miaka mitano kwa kila afisa.Walipa ushuru wa Kenya katika kipindi cha 2013-2018 watatumia kiasi kikubwa cha fedha kwa kulipa zaidi ya watu 2000 waliochaguliwa, kuteuliwa na kuchaguliwa kufuatia uchaguzi mkuu wa Machi 4, 2013. Hii inawajumuisha Rais na Naibu wa Rais (2); angalau Wajumbe 350 wa Bunge; angalau Wajumbe 68 wa Seneti,

6 Ripoti ya Februari 2013 ya SRC
7 Ripoti ya Uchunguzi wa Ukosefu wa Usawa
8 Mahakama kuu zaidi mnamo Desemba 2012 iliamua kuwa Kifungu cha 81(b) cha Katiba kinachosema,"si zaidi ya theluthi mbili ya viongozi katika mashirika ya umma wasiwe wa jinsia moja," na ifanywe kwa utaratibu.Hata hivyo,uamuzi huu haushurutishi Baraza la Kaunti kwa kifungu cha 77(2) kinasema,"Baraza la Kaunti litakuwa na viti maalum vya wanachama ili kuhakikisha kwamba si zaidi ya theluthi mbili ya wanachama kwa Baraza wawe wa jinsia moja"

Magavana 47,Naibu wa Magavana 47 na  Spika 47 wa Mabaraza za Kaunti; na angalau Wawakilishi 1450 wa Wadi katika Bunge la Kaunti. Hii ni idadi ndogo kabisa kwa sababu,  kutochaguliwa kwa uchaguzi wanawake yamaanisha kutakuwa na uteuzi, ili kupata theluthi mbili[8] ya jinsia hasa katika Baraza la Kaunti, ambapo sheria hii itatumika mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2013.

Kwa mujibu wa Tume ya Mishahara na Malipo (SRC)[9], makadirio ya ujira Kenya yamechukua zaidi ya asilimia 35% ya ushuru / mapato yaliyokusanywa kila mwaka na ni juu ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika (asilimia 29.5%); Bara Asia (asilimia 23.1%) na Umoja wa Ulaya (asilimia 16.3%). Ijapokuwa mapitio yamependekezwa, bado ni muhimu kuhakikisha kwamba wote waliochaguliwa na walipa ushuru wana ufahamu wa ubora wa kazi wanaopaswa kutarajia kutoka kulipa kiasi kikubwa na  kufuatilia mara kwa mara utendaji ili kupata thamani ya fedha zao.

| Ofisi ya Kuchaguliwa | MAPENDEKEZO YA MISHAHARA KILA MWEZI | | JUMLA KWA MWAKA(CHINI) | JUMLA YOTE KWA NAFASI ZA WALIOCHA-GULIWA | JUMLA YA YOTE WALIOPOKEA KWA MTU MMOJA KWA | JUMLA YA WALIYOPOKEA KATIKA NAFASI ZOTE KWA MIAKA TANO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | MINIMUM | MAXIMUM | | | | |
| 1.Rais(1) | 1,237,500 | 1,650, 000 | 14,850,000 | Ksh 14,850,000 | Ksh 74,250, 000 | Ksh 74,250,000 |
| 2.Naibu Rais(1) | 1,115,625 | 1,487,500 | 13,387,500 | Ksh 13,387,500 | Ksh 66, 937, 500 | Ksh 66,937, 500 |
| 3.Spika wa Baraza la Kitaifa(1) | 990,000 | 1,155,000 | 11,880,000 | 11,880,000 | 59,400,000 | Ksh 59,400,000 |
| 4. Naibu Spika wa Bunge la Kitaifa (1) | 792,000 | 1,056,000 | 9,504,000 | Ksh9,504,000 | Ksh47,520,000 | Ksh47,520,000 |
| 5.Mbunge wa Bunge la Kitaifa (Angalau 349) | 532,500 | 710,000 | 6,390,000 | Ksh6,390,000 | Ksh31,951,000 | Ksh11,150,900,000 |
| 6.Spika wa Seneti (1) | 1,237,500 | 1,320,000 | 14,850,000 | 14,850,000 | 74,250,000 | Ksh 74,250,000 |
| 7.Naibu Spika wa Seneti (1) | 990,000 | 1,056,000 | 11,880,000 | 11,880,000 | 59,400,000 | Ksh 59,400,000 |
| 8.Mjumbe wa Seneti (67) | 532,500 | 710,000 | 6,390,000 | Ksh6,390,000 | Ksh31,951,000 | Ksh2,140,717,000 |
| 9.Gavana (47) | 640,681 | 854,241 | 7,688,172 | 7,688,172 | 38,440,860 | Ksh1,806,720,420 |
| 10.Naibu Gavana(47) | 461,250 | 615,000 | 5,535,000 | 5,535,000 | 27,675,000 | Ksh, 1,300,725,000 |
| 11.Spika wa Baraza la Kaunti (47) | 225,000 | 00,000 | 3,600,000 | 3,600,000 | 18,000,000 | Ksh 846,000,0000 |
| 12. Mjumbe wa Baraza la Kaunti(Angalau 1450+ 772 wajumbe wateule) | 180,000 | 240,000. | 2,160,000 | 4,799,520,000 | 23,997,600,000 | Ksh 23,997,600,000 |

*Asili: Tume ya Mishahara na Marupurupu(SRC),Notisi ya Gazeti la Serikali Nambari.2885,2886,2827 na 2888 Marupurupu na faida ya Maafisa wa Serikali katika Serikali Kuu,tarehe 2 Februari 2013 na ilianza,Machi 1,2013- Imerekebishwa tarehe 28 Septemba 2013*

Uchunguzi[10] umeonyesha kuwa wapiga kura ambao hufurahi kuadhimisha ushindi na kuja katika ofisi za viongozi waliowapigia kura kwa mara nyingi hawaridhishwi na utendaji kazi wao kadri ya  miezi 3-6 baada ya uchaguzi mkuu. Hii inaibua maswali kuhusu ya kutoridhishwa kwa watu kama wapiga kura, tu miezi 3-6 kabla  walikuwa na shauku na kuamini wanaweza kufanya kazi hiyo waliochaguliwa kufanya. Inawezekana kuwa sababu  ni kutoelewa  jukumu la waliochaguliwa maafisa wanatarajiwa kutenda dhima ipi?

9 Tume ya Mishahara na Malipo,Uamuzi wa Malipo wa maafisa wa serikali Kenya,Februari 2013
10 Uchunguzi wa IPSOS Machi 2014 wa Utendaji wa Serikali ya Jubilee



Sehemu inayofuata inaeleza kwa ufupi dhima-kazi muhimu,majukumu na maelezo ya kazi ya kila maafisa wa serikali waliochaguliwa.



# 2.0 Kanuni ya Mgawanyo wa Madaraka



*Bunge kongwe duniani linapatikana Iceland(Althing) lililoketiwa mara ya kwanza karne ya kumi tarehe Juni 23,0930. Asili:Wikipedia*

Aina ya kwanza ya serikali ililimbikizia mamlaka katika mtu mmoja; Mfalme dhahiri. Huyu mtu alikuwa mkuu wa serikali, kuongoza majeshi ya taifa lake na maoni yake binafsi kimsingi yalikuwa sera ya taifa ya kigeni. Mfalme dhahiri pia alikuwa mkuu wa kutengeza sheria (bunge) ambaye maoni yake na ya wale walio karibu naye kuamua nini ilikuwa sheria au kinyume cha sheria, alijaribu wahalifu na kuamua ambaye alikuwa na hatia au wasio na hatia na ni adhabu ipi inapaswa kutolewa kwa wale waliopatikana wamevunja sheria. Mfalme dhahiri pia alikuwa mkuu wa wasii / Utekelezaji. Yeye aliamua ushuru gani unapaswa kulipwa na jinsi unafaa kukusanywa na nani. Mfalme dhahiri pia aliashiria nani anafaa kuajiriwa katika vikosi vya jeshi au polisi na kuamua kama wanapaswa kulipwa na kiasi gani. Wale wote waliofanya kazi kwa watawala na kwa ugani kwa taifa pia walipeana taarifa moja kwa moja au kwa wale alikuwa amewachaguwa binafsi. Jukumu la wananchi katika ufalme dhahiri lilikuwa kulipa ushuru na kutii sheria bila ya kuhoji au kulalamika kuhusu mwenendo wa viongozi wao.

Bila mshtuko, matumizi mabaya ya madaraka wa uongozi dhahiri ilikuwa kama jambo la kawaida, mara nyingi kupitia ushawishi wa wale walio karibu na mfalme. Maandiko mbalimbali ya kihistoria ikiwa ni pamoja na Biblia inaelezea mifano mingi ya matumizi mabaya ya madaraka katika hadithi kama vile maamuzi ya sheria ambayo yalihitaji wananchi wote kuabudu mfalme na wale wasiofuata kuadhibiwa kwa njia ya mauti katika kuwekwa kwa pango la simba, au kukatwa kichwa. Wengi pia walikufa katika magereza.

Leo hii, neno 'Mfalme Dhahiri' ambaye mara nyingi hakuchaguliwa lakini kurithi kiti chake cha enzi imebadilishwa na neno 'dikteta' ambayo inakamata mkusanyiko huo wa mamlaka kwa mtu mmoja, tofauti tu ni kuwa mara nyingi madikteta huja mamlakani kupitia uchaguzi na mara nyingi huwa maarufu kabisa wakati wa uchaguzi na hivyo maneno yao huwa na ushawishi mkubwa juu ya mwenendo wa kitaifa. Mfano ni Ujerumani wakati Adolf Hitler alipoingia mamlakani kwa njia ya uchaguzi na alikuwa maarufu sana mwanzoni mwa utawala wake. Hata hivyo, kwa sababu ni rahisi sana kwa wananchi kuwacha kiongozi maarufu kuendesha shughuli zake bila kuchunguza, ni mara nyingi viongozi hao kwa urahisi kuwa madikteta kama hakuna mfumo wa wazi wa kuangalia mamlaka yao au kama mfumo si madhubuti kuzingatiwa.

Baada ya maelfu ya miaka ya kujaribu aina mbalimbali za serikali, imekuwa wazi kwamba mkusanyiko wa mamlaka kwa mtu mmoja unaweza kufanya watu wazuri wawe viongozi wabaya au kuwafanya kuacha urithi usio wa haki, uongozi mbaya ambo utafanya taifa lolote kuwa maskini kwa sababu wasaidizi wake wanatumikia mamlaka vibaya kwa jina la kiongozi kabisa.Kiongozi wa Uhabeshi Haile Selassie ni mfano wa karibuni wa Afrika. Utambuzi huu unaonyeshwa bora kwa msemo "Mamlaka huchanganya na mamlaka kabisa huharibu".

Majukumu ya serikali ni mengi na tofauti. Ni muhimu kugawa kazi hizi miongoni mwa matawi maalum, hivyo kuwa jukumu la kufanya liwe wazi na haisababishi mkusanyiko wa mamlaka katika tawi moja. Mgawanyo wa madaraka ya kiserikali chini ya katiba yoyote hufanyika katika njia mbili - wima na mlalo..

Historia ya Kenya inatambua kuwa mabadiliko mengi yaliyofanywa katika Katiba ya uhuru yalisababisha mkusanyiko wa madaraka katika urais. Kwa hivyo Katiba ya Kenya, 2010 inasisitiza kanuni ya mgawanyo wa madaraka na inataka kuepuka kabisa kuzingatia mamlaka katika kituo kimoja au mtu.

Katika Katiba ya Kenya, 2010, kupunguza mamlaka ya kifalme dhahiri au dikteta yamefanikiwa kwa kutawanya mamlaka kimlalo kwa matawi matatu ya serikali; Bunge, Serikali-Mtendaji na Idara ya Mahakama katika Kenya. Hii ni dhana maalumu katika Kenya kwa sababu ilikuwepo katika Katiba ya uhuru. Hata hivyo, kwa sababu ilikuwa ikitumika sana vibaya na kupuuzwa katika miaka hamsni ya uhuru wa Kenya,kuna hitajika kufanywa elimu ya uraia juu ya matumizi yake bora.

Katiba imetumia chombo au mfumo uitwao ugatuzi kugawanya madaraka wima kwa kujenga ngazi mbili za serikali - ya taifa na kaunti.

Kifungu cha 6 (2) cha Katiba kinasema kwamba "serikali katika ngazi ya kitaifa na kaunti ni tofauti na baina ya tegemezi na zitafanya uhusiano wao juu ya msingi wa mashauriano na ushirikiano." Kifungu cha 191 ambacho kinaauni migogoro kati ya kaunti na serikali za kitaifa kinaweka wazi kwamba serikali ya kaunti haiko chini ya serikali ya kitaifa. Hii ni kupitia njia ya kwamba kifungu cha 191 (4) kinatafakari na kutambua kwamba kuna wakati ambapo sheria ya kaunti itakuwa ipo juu ya sheria za kitaifa.

Ushauri na ushirikiano pia ni muhimu kupitia ukweli kwamba mabunge ya kaunti yatakuwa yakitunga sheria ambayo itakuwa inatekelezwa katika ngazi ya kaunti. Ili kufanya hivyo, kutakuwa na haja ya kujenga uwezo kwa ajili ya mashtaka kwa ukiukaji wa sheria ya kaunti. Hii inaleta haja ya kushauriana kati ya kaunti na Kiongozi wa Mashtaka (DPP) na hata ikiwezekana kufanyika majadiliano kwa ajili ya uhamisho chini ya kifungu cha 187 ya kazi ya kuendesha mashtaka kama itapatikana, kazi hizi ni bora kufanywa na serikali ya kaunti. Uhamisho bado una maana kwamba udhibiti hatimaye bado utakuwa wajibu wa DPP.

## 2.1 Vithibiti na Visawishaji Kupitia Matawi Matatu ya Serikali

Katiba ya Kenya inatekeleza kanuni ya mgawanyo wa madaraka kwa mlalo na wima.Inagawanya madaraka wima kwa kukabidhi ugatuzi ambao unajenga ngazi mbili za serikali - ya taifa na kaunti.

Mlalo, serikali ina matawi tatu kila moja ikiwa na kazi maalum - Bunge ambalo huunda sheria na hasa sheria za matumizi ya mapato ya kitaifa;Serikali-Mtendaji ambayo hutekeleza sheria ilioidhinishwa na matumizi ya bajeti yaliopitishwa kama sheria na bunge; na Mahakama, ambayo inasuluhisha migogoro na kutafsiri sheria[11]. Kila tawi lina mamlaka tofauti na huru na maeneo ya uwajibikaji hivyo kwamba hakuna tawi lina mamlaka zaidi kuliko tawi lingine.Kila tawi huthibiti na husawisha tawi lengine.

Bila mfumo wa vithibiti na visawishaji kila taasisi itaweza kuwa na madaraka mingi; sheria kwa yenyewe na katika mchakato wa kukandamiza wengine katika matawi mawili kurudia katika kifalme kabisa au udikteta. Mgawanyo wa madaraka unahakikisha kwamba kila tawi liko na mamlaka kikatiba juu ya lengine.

Kwa mfano, mtendaji rasimu ya bajeti ya kitaifa na mawaziri lakini hawawezi kutumia mapato ya taifa kutekeleza bajeti hii mpaka bunge kuidhinisha bajeti kwa kupitisha Makadirio ya Matumizi kuwa sheria ambayo inaruhusu matumizi. Kwa njia hii, tawi la sheria huangalia ni jinsi gani serikali inatumia ushuru wa watu wake. Hii ina maana kwamba serikali-mtendaji (Mamlaka ya Mapato Kenya, wizara na serikali kaunti wanaokusanya ushuru kwa mfano ingawa ushuru, leseni,gharama ya huduma nk) hawezi kukusanya kodi na kutumia mapato haya bila kuangaliwa bungeni kwa kupitia mswada wa matumizi huo na njia nyingine kama vile Mdhibiti wa Bajeti, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Kamati ya Umma ya Hesabu ya bunge nk kwamba kushikilia serikali-mtendaji kuwajibika kwa ajili ya matumizi ya rasilimali za serikali.

Mfano mwingine wa matawi matatu ya serikali kuhudumia kama vithibiti na visawishaji juu ya kila moja ni wakati bunge inapiga kura kuanzisha kesi za kinidhamu dhidi ya wanachama wa Tume ya Huduma ya (JSC) (mahakama) na rais - mtendaji huwa na tume ya kuchunguza nidhamu za majaji. Au wakati bunge hupiga kura kupanua au mamlaka ya mahakama au ya rais. Vile vile wakati mahakama hufanya maagizo kuelekezwa dhidi ya mtendaji na mahakama kama mfano wakati mahakama inatangaza kupitia ilani ya gazeti kwamba SRC ni kinyume na katiba, kwamba si kuingiliwa na kazi ya tawi lengine lakini ufunuo muhimu ya mfumo wa vithibiti na visawishaji. Yote haya ni udhihirisho wa mafundisho ya mgawanyo wa madaraka.

Chini ya Katiba ya Kenya, 2010 matawi ya serikali la wabunge na serikali-mtendaji sasa iko katika ngazi mbili - Kitaifa na Kaunti. Hii ina maana kwamba maafisa nane wa serikali waliochaguliwa kufuatia uchaguzi wa Machi 2013, nne, yaani Rais, Naibu Rais na Gavana na Naibu Gavana kutumikia katika tawi la Mtendaji wa serikali, wakati wengine wanne kutumikia katika tawi la wabunge wa serikali yaani Mwakilishi wa Eneo Bunge (MP) na mwakilishi wa wanawake wa Bunge la Taifa, Seneta na Mwakilishi wa wadi katika Bunge la Kaunti (Mwakilishi wa Kaunti).

Kazi na wajibu ya wale wanaohudumu katika Serikali-Mtendaji ni tofauti na wale waliochaguliwa viongozi wa kuwahudumia katika Bunge. Muhtasari huu unaeleza kwa kifupi: -

i) kazi kwa ujumla na majukumu ya wabunge wanne waliochaguliwa katika Kenya; kisha inaelezea tofauti kidogo katika majukumu ya mbunge hutekeleza.

ii) kazi maalum na majukumu ya Rais na makamu wa rais, ni tofauti na jukumu la Gavana na naibu wa gavana, ambaye hutumikia katika serikali ya kitaifa na ya kaunti mtawalia.

11 Mwanafilosofia Baron Montesquieu wa Ufaransa alisisititiza mamlaka mingi yakiwa sehumu moja ni hatari na yanaweza leta ukatili kwa serikali.Ametambulika kama mwanzilishi wa nadharia ya kutenganisha mamlaka.



## 2.2 Kazi Muhimu za Watunga Sheria wote - Kikanda, Kitaifa, Seneti na Bunge la Kaunti

Mojawapo ya mabadiliko makubwa ambayo Katiba ya Kenya 2010 ilileta ni katika ufafanuzi na muundo wa 'Bunge'. Kifungu cha 93 (1) kinasema kwamba Bunge la Kenya sasa liko mara mbili; Bunge na Seneti. Hii ina maana kwamba neno 'Mwakilishi Bungeni' au Mbunge sasa inamaanisha maafisa wote waliochaguliwa ambao hukaa katika Bunge la Taifa na Seneti.

Katika ngazi ya kitaifa, tawi la uundaji sheria lina maana ya Bunge la Kitaifa na Seneti. Kenya iko katika Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC) ambalo pia lina matawi matatu ya serikali – Serikali utendaji, Bunge na asasi ya Mahakama. Wabunge ambao wapiga kura huchagua katika Bunge la Kenya ndio wanaoteua wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA). Hii ina maana kwamba uchaguzi wa watu kitaifa kwa ujumla una ushawishi mkubwa kwa upande wa Kenya katika ngazi ya kikanda.

Katika ngazi ya kaunti, tawi la wabunge serikalini linahusu wawakilishi kutoka kila wadi kuhudumia Bunge la Kaunti katika kila moja ya Kaunti 47. Kwa hivyo neno watunga sheria linahusu wote waliomo si tu katika nyumba tatu bali- Seneti, Bunge na Bunge la Kaunti, lakini pia wanasheria waliochaguliwa na vyama vya kisiasa katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA).

Katiba ya Kenya, mwaka 2010 ikosambamba na viwango bora vya kimataifa kubainisha kazi muhimu nane katika ngazi ya kitaifa na Kaunti na jinsi wanapaswa kufanya ambayo pia kwa kiasi kikubwa ni sawa na wale wanachama wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), ila kwa tofauti zinazotokana na ngazi za serikali. Na ubaguzi wa jukumu la sita, ambayo inatumika tu katika ngazi ya kitaifa na wabunge, majukumu mengine saba yanatekelezwa na wabunge wote, na Wawakilishi wa Kaunti katika Baraza la Kaunti kuangalia utendaji na wanaweza kuondoa gavana kutoka afisini, wakati Bunge huangalia utendaji wanaweza kumuondoa Rais madarakani, wakati wabunge wa EALA lazima waangalie serikali za jumuia.

Kimataifa[12] , kuna kazi sita[13] muhimu ambazo watunga sheria katika kila ngazi lazima wafanye. Hizi ni: -

1. **Uwakilishi[14]: Wabunge** wana wajibu wa kuwakilisha watu, yaani; kusikiliza na kueleza mapenzi ya watu katika Bunge. Kwa kufanya hivyo, wabunge lazima: -

- Kusikiliza watu; kujumuika mara kwa mara na vikundi mbalimbali wanavyowakilisha kujua maoni yao juu ya masuala mbalimbali.
- **Maslahi maalum: Usawa / Kutobagua:** watu wa Kenya si sawa; wala Kaunti 47. Mahitaji ya wanawake wote, au watu wote maskini, wachache au watu wanyonge si sawa. Wabunge wote wana wajibu wa kuhakikisha kuwa mahitaji mbalimbali ya makundi tofauti wanayowakilisha yanashughulikiwa katika utoaji wa maamuzi, sheria na bajeti. Hasa wawakilishi wa wanawake na wabunge katika Bunge ambao huwakilisha maslahi maalum lazima wasimame wima katika kuhakikisha mahitaji ya wale wanaowakilisha yanashughulikiwa.
- Kueleza mahitaji ya wananchi kwa taasisi zenya kutekeleza jukumu flani.
- Wapatikane kwa urahisi na daima kutenda maslahi ya watu wote ndani ya nchi na kimataifa.
- Wahakikishe kwamba yanayotendeka bunge ni wazi kwa umma na vyombo vya habari.
- Wahakikishe kwamba wananchi daima wajua nini mbunge wao hufanya, msimamo au maoni yake juu ya maswala muhimu na ni kwa nini.

12 Ona faharasa ya Bunge la Africa na Uchunguzi wa Uwazi wa Bajeti,2012 inayopatikana www.parlcent.org/en/...API-African-Parliamentary-Index.pdf iliyoangaliwa Machi 14,2013
13 Vifungu 3(a) na 95(2) vya Katiba ya Kenya
14 Vifungu 94(5-6) na 2(5) vya Katiba ya Kenya

2. **Sheria:** Watunga sheria wana wajibu wa kutunga sheria kwa kutafiti, kwa kuzingatia, mjadala kisha kupitisha miswada iliyoletwa na serikali ya kitaifa au watu binafsi. Wanaweza pia kufuta au kufanya marekebisho ya sheria. Baadhi ya mambo muhimu kuhusu watunga sheria ni wajibu na uwezo wa kufanya sheria pamoja na: -

- **Mapatano ya kimataifa na Mikataba:** Watunga sheria wana wajibu wa kuidhinisha au kuzuia serikali kuu kuingia katika mapatano ya kimataifa / mikataba ambayo haijali maslahi ya Wakenya.
- **Sheria zinazofuata sheria ya kimataifa:** Chini ya Kifungu 2 (5), Bunge lina jukumu la kuunda sheria ili kuwezesha kufuata sheria za kimataifa na ahadi Kenya imeingia ndani, mfano Maendeleo ya Milenia (MDGs); Sheria ya Urumi na kadhalika.
- **Marekebisho ya katiba na Mipaka ya Kaunti:** Bunge inaweza kufikiria na kupitisha marekebisho ya Katiba ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya mipaka ya Kaunti lakini tu kama vile marekebisho yanazingatia maslahi ya watu ikiwa ni pamoja na vikundi maalum; na izingatie Katiba-Kifungu cha 94 (3).
- Watunga sheria lazima wawajibike kwa sababu wao wana uwezo wa kumpinga Rais kisheria. Chini ya kifungu cha 115 (4) cha Katiba, mswada ambao Rais ameelezea kutoridhishwa bado unaweza kuwa sheria bila kutiwa saini na Rais kama theluthi mbili ya Bunge na theluthi mbili ya Seneti wapiga kura kwa mswada huo kuwa sheria bila ya kujali kutoridhishwa kwa Rais. Zaidi ya hayo, mswada ambao umepitia matakwa ya kikatiba yote kuwa sheria hata kama Rais hatatia sahihi ndani ya siku saba baada ya kuwasilishwa kwake.
- Kuundaa sheria ya jinsi gani serikali itaongeza fedha kutokana na ushuru na kupitisha matumizi ya serikali

3. **Nguvu za mfuko wa fedha na Usimamizi wa Fedha.** Watu wa Kenya wanafadhili serikali kupitia ushuru[15].

